# 14 UDANGANYIFU MBAYA ZAIDI KATIKA HISTORIA



Udanganyifu umetapakaa katika kila nyanja za jamii. Huu tunaukuta katika sayansi, katika uchumi wa sanaa, uandishi, na penginepo. Kwa bahati mbaya, pia kuna udanganyifu katika mambo ya kidini. Udanganyifu mbaya zaidi wa vizazi vyote ni ule wa desturi za kipagani za ibada ya mungu jua ambayo kwa ujanja imechomekwa katika Ukristo, kwenye kiwango cha kuingiza ibada ya jua badala ya ile ya zile Amri Kumi.

Ibada ya jua ni ya zamani kabisa. Mithras, Aurora, Marduk, Baal, Ra, Osiril na Shamas walikuwa ni miungu walioliwakilisha jua.

## *IBADA YA JUA ILIYOGEUZWA*

**1. Je, ni machukizo gani ambayo nabii Ezekieli aliyaona katika maono? Ezekieli 8:15-18.**

________________________________________________________________________

Mungu alitamka hukumu kali kabisa juu ya waabudu jua (Ezekieli 6:4-6).

**2. Je, ni nani aliyejaribu kuleta desturi za kipagani katika Ukristo? Kwa nini?**

*Mfalme Konstantino (mwaka 280-337B.K.) aligundua ya kwamba nguvu za kisiasa za Rumi zilikuwa zinadhoofu kutokana na tofauti zilizokuwa zinajitokeza kati ya waabudu upagani na Wakristo. Ndipo akathubutu kuyaleta makundi haya mawili makubwa pamoja. Mnamo 313 B.K., alichapisha ile Sheria ya Milano, ambayo ndani yake alileta ustahimilivu wa kidini na uhuru kamili kwa Wakristo.*

*Matokeo yake, walionesha heshima kubwa kwa Mfalme huyu. Wapagani waliabudu miungu mingi, Mithraso akiwa ni mmoja wapo wa mungu jua wakuu.*

*Mathraso aliabudiwa panapo Jumapili. Hata leo, siku ya kwanza ya juma katika Kingereza ni Sunday, na katika Kijerumani ni Sonntag, yote yakimaanisha siku ya jua yanapofasiriwa.*

*Ili kuitimiliza agenda hii ya kisiasa, Konstantino mwenyewe akaingia katika Ukristo na akainzisha Jumapili, siku ya jua, kama siku ya kupumzika, badala ya Sabato iliyoadhimishwa na Wakristo waaminifu, jinsi hii alikidumisha kiunganishi pamoja na waabudu jua.*

*Wengi wakawa "Wakristo" na kuleta idadi kubwa ya desturi za kipagani katika Ukristo. Kadinali John Henry Newman katika kitabu chake "Development of Christian Doctrine" (Maendeleo ya Mafundisho ya Kikristo), uk. 373 anasema: "Eusabius anatueleza sisi ya kwamba Konstantino, anapoipendekeza dini hii mpya kwa wapagani hawa, akihamishia huko yale madoido ya nje ambayo wapagani hawa wameyazowea katika madhehebu zao; matumizi ya vihekalu vilivyowekwa wakfu kwa watakatifu maalumu, mapambo yalifanyizwa katika nyakati fulani kutokana na matawi ya miti, ubani, taa mbali mbali, mishumaa, sadaka za nadhiri kwa ajili ya kuponywa kwa wagonjwa, maji matakatifu, sikukuu za majira, matumizi ya kalenda, maandamano, kubariki mashamba, mavazi ya makuhani, pete za ndoa, desturi za kukabili mashariki, na baadaye sanamu za watakatifu, pengine na nyimbo za kikanisa na ile "Kyrie Eleison" (Bwana utuhurumie), desturi hizi zote zikiwa na asili yake katika upagani na zikiwa zimetakaswa pale zilipopokelewa na kanisa."*

*The Encyclopedia Britannica (toleo la 9) katika mada ya "Jumapili" inaeleza: "Kutambuliwa kwa awali zaidi kwa kuadhimishwa kwa Jumapili kama wajibu wa kisheria ni katiba ya Konstantino mnamo 321 B.K. (Machi 7) akieleza ya kwamba mahakama zote za sheria, wakazi wa mijini, pamoja na karakana zilipasa kuwa katika pumziko panapo Jumapili kukiwa na kuachiliwa kwa wale wnaojihusisha na kazi za kilimo."*

**3. Konstantantino alikuwa ni mfalme tu, sasa uadhimishaji wa Jumapili uliingizwaje ndani ya kanisa?**

*Badiliko la siku ya pumziko lilipokelewa na Kanisa la Roma. Katekisimo iliyopokea baraka za kitume za Papa Pius X (Januari 25, 1910) zikifafanua kama ifuatavyo:*

- Swali: Siku ya pumziko ni ipi?
- Jibu: Jumamosi ndio siku ya pumziko.
- Swali: Je, ni kwa nini tunaiadhimisha Jumapili badala ya Jumamosi?
- Jibu: Tunaiadhimisha Jumapili badala ya Jumamosi kwa sababu Kanisa Katoliki, katika Sinodi ya Laodikia (mwaka 336), lilihamisha yale maadhimisho kutoka Jumamosi kwenda Jumapili. Peter Geiermann, The Convert's Catechism of the Catholic Doctrine, (Katekisimo ya Waongofu wa Mafundisho ya Wakatoliki) 1964 uk. 50.

## *JE, MUNGU ANARUHUSU SHERIA YAKE KUBADILISHWA?*

**4. Je, kutatokea nini kwa ye yote anayethubutu kuibadili sheria ya Mungu? Ufunuo 22:19.**

____________________________________________________________

**5. Je, ni kitu gani ambacho hakiruhusiwi kufanyika katika Sheria Takaifu ya Mungu? Muhubiri 3:14.**

____________________________________________________________

a) Mungu hawezi kuibadili sheria Yake. Malaki 3:6; Yakobo 1:17.

b) Sheria ya Mungu itadumu kwa vizazi elfu. Kumbukumbu 7:9.

c) Ni kweli kwamba Amri Kumi ziliandikwa kwa kidole Chake Mungu Mwenyewe katika zile mbao mbili za mawe (Kutoka 20:8-11) ikionesha juu ya umuhimu na kutotanguka kwake.

d) Ile amri inayotueleza kwamba tuishike Sabato kama siku ya pumziko ni amri ya nne ya ile Sheria Takatifu. Kutoka 20:8-11.

**6. Je, Yesu aliibadili sheria ya Mungu ama siku ya kupumzika? Mathayo 5:17, 18.**

*Yesu alisema:* __________________________________________________

**7. Kwa kulingana na unabii wa Danieli, ile mamlaka ya kibinadamu ingejaribu kufanya nini juu ya sheria ya Mungu? Danieli 7:25.** ____________________________________

*Kanisa linaamini ya kwamba linayo mamlaka ya kufanya hivyo. Stephen Keenan, Kasisi Mkatoliki, aliandika: "Laiti kama (kanisa) lisingekuwa na mamlaka kama hayo, lisingeweza kufanya kile ambacho wanadini wote wa kisasa wanakubaliana naye; lisingeweza kubadili uadhimishaji wa Jumapili-siku ya kwanza ya juma, mahali pa kuiadhimisha Jumamosi-siku ya saba ya juma, badiliko ambalo halina mamlaka ya Kimaandiko." A Doctrinal Catechism, uk. 74.*

## *JE, MISTARI HII NANE INAYOITAJA SIKU YA KWANZA YA JUMA, INATAJA BADILIKO KATIKA ILE SIKU YA PUMZIKO?*

**8. Kwani mistari hii mitano kuhusu ule ufufuo, uliotokea siku ya kwanza y juma, inataja badiliko lo lote la siku ya kupumzika? Mathayo 28:1; Marko 16:1,2; 16:9; Luka 24:1; Yohana 20:1.**

____________________________________________________________

**9. Je, ni kwa nini wale wanafunzi walikutanika siku ya kwanza ya juma? Yohana 20:19.**

*Ni kwa sababu walikuwa wanawaogopa* ____________________________________

*Ushahidi zaidi ya kwamba hawakukusanyika ili kuiadhimisha Jumapili kwa heshima ya kule kufufuka ni kuwa hata hawakuamini ya kwamba Kristo alifufuka. Marko 16:12-14.*

**10. Je, ni kwa sababu gani Paulo alirefusha huduma kule Troa, katika usiku wa siku ya kwanza ya juma? Alifanya nini katika siku iliyofuata ilipopambazuka? Matendo 20:7, 11.**

________________________________________________________________________

a) Katika Biblia, siku mpya huanza pale jua linapokuchwa, sio katika usiku wa manane, na ndivyo ilivyokuwa ya kwamba haya yalikuwa ni baada ya Sabato. Mistari mengi inaonesha ya kwamba Paulo aliabudu panapo Sabato; lakini katika tukio hili maalumu, maadamu alipasa kuondoka panapo mapambazuko, alirefusha hotuba yake hata usiku wa manane.

b) Kama Paulo angeiadhimisha Jumapili, asingefanya safari hiyo ndefu katika siku hiyo. Badiliko la siku ya pumziko haijatajwa hapa.

c) Waliumega mkate kila siku (Matendo 2:46).

**11. Katika kuwashauri kujiwekea kando sadaka kwa maskini kule Yerusalemu, je, Paulo aliwaeleza wale ndugu kukusanyika ama kujiwekea kando ile pesa? 1 Wakorintho 16:2.**

________________________________________________________________________

*Haisemi cho chote juu ya badiliko la siku ya pumziko.*

## *HAPANA HATA MSTARI MMOJA WA BIBLIA UNAOONESHA YA KWAMBA SIKU YA KWANZA YA JUMA INAPASA KUADHIMISHWA*

Hebu na tuangalie nukuu chache muhimu:

- Kadinali Gibbons aliandika: “Waweza kusoma Biblia kutoka Mwanzo hadi Ufunuo, na HUTAPATA MSTARI HATA MMOJA UNAOIDHINISHA KUTAKASWA KWA JUMAPILI. Maandiko yanakazia maadhimisho ya kidini ya Jumamosi, siku ambayo sisi wala hatuitakasi.”-The Faith of Our Fathers, toleo la 1917, uk. 72, 73.
- “Jumla ya wazo la kubadilisha siku ya kwanza ya juma mahali pa siku ya saba ya juma na kule kupisha, pengine katika namna ya kiroho, juu ya pumziko la Sabato lililosimama katika amri ya nne WALA HALIKUSIMAMA KATIKA MAANDIKO MATAKATIFU WALA KATIKA UKRISTO WA KALE.” Smith and Cheatham, Dictrionary of Christian Antiquities, mada ya Sabato.
- Dr. Edward T. Hiscox, mwandishi wa Kanuni ya Wabaptist (Baptist Manual) alitoa tamko lifuatalo mbele ya kundi la wachungaji: “Kulikuwako na iko amri ambayo yapasa kuadhimishwa kama takatifu: hii Sabato, lakini siku ile ni Jumamosi na wala sio Jumapili. Kwa hiyo, yaweza kusemwa, ya kwamba Sabato ilihamishwa kutoka kwenye siku ya saba hadi kwenye siku ya kwanza. Ni wapi kule ambako usajili wa badiliko kama hili waweza kupatikana? Wala hakuna katika Agano Jipya, maadamu hakuna kabisa kinachohusiana na jambo hili.” Kutoka kwenye kipengee kilichosomwa katika Mkutano huo wa Wachungaji kule New York, panapo Novemba 13, 1893.

## *MASWALI FULANI KUHUSU SABATO*

**12. Tunawezaje kufahamu kama Sabato hii ya leo ndio ile ambayo Mungu aliitakasa katika uumbaji? Je, hakujawa na badiliko katika kalenda?**

a) Tukiangalia katika kalenda ya Wakristo, Wa-orientali, Waislamu, Wakoptiki ama Wayahudi, tunaona kuwa miaka inabadilika, lakini Sabato inasalia kuwa ile ile. Katika kalenda ya Kiyahudi, mwaka 5778 ni sawa na mwaka wetu wa 2018.

b) Kalenda ya Juliani ilianza kunako mwaka 46 K.K. ikaja kusahihishwa mnamo 1582 na kubadilishwa jina kuwa ni kalenda ya Gregori; hii ndio tunaitumia hata leo.

Pale wataalamu wa elimu ya nyota walipogundua ya kwamba majira ya machipuo huanza katika nyakati tofauti; tarehe za kalenda zilisogezwa kwa siku 10 mbele, ilikuwa ni Alhamisi, Oktoba 4, watu walipokwenda kulala usiku na walipoamka siku ya Ijumaa ilikuwa ni Oktoba 15. Mzunguko wa juma haukubadilika.

c) Kuna vipande viwili vya ushahidi unaoonesha kwamba Sabato ni ile ile iliyotajwa katika uumbaji:
   1. Ule mujiza wa mana kule jangwani. Mungu anaijua ile siku aliyoitakasa. Mungu aliwapa kiasi mara dufu ya mana panapo Ijumaa na asiwape cho chote panapo Sabato (Kutoka 16:4-35). Mungu alifanya mujiza huu jangwani yapata mara 2000.
   2. Kristo pamoja na wanafunzi Wake walitunza Sabato (Luka 4:16; 23:54-56). Je, Mwana wa Mungu alitunza siku potofu kwa miaka 33?

**13. Paulo anaelezea juu ya Sabato gani anayoitaja katika Wakolosai 2:16, 17: siku za mapumziko zilizoamriwa, ambazo zilikuwa ni kivuli cha Kristo, ama ni ile siku ya saba?**

____________________________________________________________

*Katika ile sheria ya maadhimisho, iliyoandikwa na Musa katika kitabu (Kumbukumbu 31:24-26), kuna sikukuu saba za mwaka, ambazo zilitokea katika mwezi wa kwanza na wa saba. Sikukuu hizi (Pasaka, sikukuu ya Mkate Usiotiwa Chachu, Malimbuko, Pentekoste, Sikukuu ya kuzipiga Baragumu, Siku ya Upatanisho, na Sikukuu ya Vibanda) hizi zote ziliitwa pia ni Sabato ama siku za mapumziko. Hazikuwa na uhusiano na ile amri ya nne (Walawi 23:38, 39). Zilikuwa ni kivuli ama mfano wa Kristo.*

**14. Je, suala hili ni muhimu kiasi hicho? Je, haiwezi kuwa sawa ukiitunza siku nyingine yo yote? Je, tunaweza kuyatumainia maoni yetu? Mithali 16:25.**

____________________________________________________________

**15. Watu wengi huiadhimisha Jumapili; je, watu hao wengi waweza kukosea? Ni nani watakaopotea? Mathayo 7:13, 14.**

____________________________________________________________

a) Sio suala la kuungana na walio wengi ama wachache bali kuwa upande wa Yesu.

b) Watu wengi husema: “Wazazi wangu na mababu zangu siku zote wametunza Jumapili, nami sipendi kuwa tofauti.” Je, ni nani ambaye Mungu atamlaumu na kumhukumu: ni wale waliotenda dhambi kwa kutojua ama waliotenda dhambi kwa kufahamu? Matendo 17:30; Yakobo 4:17.

## HITIMISHO

**16. Je, Biblia yawaitaje wale wanaorejeza Sabato kama siku ya pumziko? Isaya 58:12, 13.**

____________________________________________________________

**17. Je, Bwana anaiitaje Sabato na ni baraka gani ambazo tunazipokea katika siku hii? Isaya 58:13, 14.**

____________________________________________________________

***Uamuzi wangu:*** *Ninakubali kwamba Sabato ya Mungu imegeuzwa kwa hila na Jumapili, siku ya ibada za kipagani na iliyobuniwa.* ◯ *Ndio* ◯ *Hapana*